CHRISTIAN COUNCIL OF TANZANIA
JUMUIYA YA KIKRISTO TANZANIA
CCT CHURCH HOUSE

Tel. 026 232 4445
026 232 1467
026 232 1770
026 232 4212
Fax: 026 232 4352

P. O. Box 1454,
Dodoma,
Tanzania.

**Tamko la Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT) Kuhusu Uchaguzi wa Serikali za Mitaa Tarehe 27 Novemba 2024**

**Ndugu Wanachama wa Jumuiya ya Kikristo Tanzania na Watanzania wote kwa ujumla**

Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT) katika kikao chake cha Kamati ya Utendaji kilichofanyika leo tarehe 14.11.2024 pamoja na mambo mengine kimejadili kwa kina hali ya kisiasa ilivyo katika Taifa letu. Baada ya tafakari hiyo CCT inapenda kutoa tamko hili kuhusiana na uchaguzi wa serikali za mitaa utakaofanyika tarehe 27 Novemba 2024. Ifahamike kuwa CCT imekua ikifuatilia kwa makini mchakato mzima wa uchaguzi huu tangu mwanzo, ikishiriki katika kutoa maoni wakati wa uandaaji wa sheria na kanuni za uchaguzi na kufuatilia maandalizi ya uchaguzi tangu ambapo Mh. Waziri mwenye dhamana ya Ofisi ya Rais TAMISEMI (OR-TAMISEMI) alipotangaza ratiba nzima ya uchaguzi chini ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa za Mwaka 2024 (Matangazo ya Serikali Na. 571, 572, 573, na 574 ya mwaka 2024).

**Changamoto Zilizobainika Katika Maandalizi ya Uchaguzi:**

1. **Malalamiko Kuhusu Daftari la Wapiga Kura:** Kumekuwa na malalamiko juu ya uandikishaji wa wapiga kura wasiokuwa na sifa, kutofuatwa kwa utaratibu na muda mfupi wa uandikishaji wa siku saba tu, hali iliyosababisha baadhi ya watu wenye sifa kushindwa kuandikishwa. Pia, baadhi ya watu kuonekana kutokidhi vigezo kwa mujibu wa sheria Mf. Majina ya watu waliokwisha kufariki bado yapo katika daftari na wengine kutokuwa na umri stahiki.
2. **Kuenguliwa kwa Wagombea kwa Sababu Ndogo za Kiufundi:** Tumebaini kuwa kumekuwa na malalamiko mengi kuhusu kuenguliwa kwa majina mengi ya wagombea kwa makosa madogo kama kushindwa kuandika majina matatu, anuani au kasoro ndogo zinazoweza kurekebishwa, jambo linalotia shaka kuhusu haki katika mchakato wa uteuzi.
3. **Vikwazo Katika Kuchukua na Kurudisha Fomu za Wagombea:** Kumewepo na malalamiko kuwa baadhi ya wagombea hususani wa vyama vya upinzani wamewekewa vikwazo, baadhi ya ofisi zimekutwa zimefungwa wakati wa kurudisha fomu, na fomu nyingi zimeshindwa kubandikwa au

zimebandikwa vibaya kilichopelekea kuharibika au kutodumu kwa muda mrefu kwenye Mbao za matangazo.

4. **Mapingamizi ya Rufaa:** Tumeshuhudia changamoto katika mchakato wa kukata rufaa ambapo siku ya kupokea rufaa baadhi ya wasimamizi walifunga ofisi na kuzuia mapingamizi mengi, jambo linalosababisha malalamiko miongoni mwa wagombea.
5. **Kutekwa, Kujeruhiwa, Kupotea na Kuuawa kwa Wananchi kunakohusiana na masuala ya siasa na uchaguzi:** Tumeendelea kushuhudia kwa siku za karibuni watu kupotea na wengine kuuawa tunapoelekea kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa. CCT inakemea vitendo hivyo na kuzitaka Mamlaka husika kufanya ufuatiliaji wa kina utakaopelekea kupatikana majibu ili kuondoa taharuki na hofu iliyopo kwenye jamii.

**Rai ya CCT kwa Wananchi, Vyama vya Siasa na Serikali Tunapoelekea Uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2024:**

1. **Kwa Wananchi:**

i. **Kujitokeza kwa Wingi Kupiga Kura:** Tunawahamasisha wananchi wote waliojiandikisha kujitokeza kwa wingi na kutimiza haki yao ya kuchagua viongozi wa kijamii wa mtaa, kijiji, na kitongoji wenye sifa sio kwa ushabiki wowote ule. Wananchi wote waendelee kudumisha amani na mshikamano wakati wote wa uchaguzi.

ii. **Kufuatilia Kampeni na Kuchagua kwa Hekima:** Ni muhimu kufuatilia kampeni kwa makini na kuchagua viongozi wanaoonekana kuleta maendeleo ya kijamii.

iii. **Kulinda Amani na Utulivu:** Tunawasihi waumini na wananchi wote kwa ujumla kudumisha amani na utulivu kabla, wakati na baada ya uchaguzi. Tunahimiza kuepuka vishawishi vyovyote vya kiitikadi au namna yoyote inayoweza kuleta machafuko katika maeneo yetu na taifa kwa ujumla.

iv. **Wito wa Maombi:** Tunahimiza waumini wote kumtanguliza Mungu mbele katika kipindi hiki muhimu tunapoelekea kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa kwa ajili ya maendeleo na ustawi wa taifa la Tanzania.

v. Ieleweke kuwa endapo mgombea hana mpinzani sheria inaelekeza apigiwe kura ya NDIYO au HAPANA ili kutoa haki kwa Wananchi kuchagua viongozi wanaowataka.

2. **Kwa Vyama vya Siasa**

i. **Kampeni:** Kufuatilia na kusimamia kampeni za wagombea kutoka katika vyama vyao na kuhimiza ustaarabu na kuheshimiana katika kunadi sera za chama husika bila kutumia lugha mbaya za matusi /maudhi zinazoweza kuhatarisha amani ya nchi yetu.

ii. **Kuhesabu, kujumlisha na kutangaza matokeo:** tunahamasisha vyama vyote vinavyowania nafasi za uchaguzi kuweka mawakala waadilifu katika kusimamia zoezi zima la upigaji kura, kuhesabu, kujumlisha na kutangaza matokeo ili kuepuka sintofahamu baada ya uchaguzi na kutupiana lawama.

3. **Kwa Serikali na Mamlaka Husika:**

Tunaipongeza Serikali kwa kupokea wito wa Wananchi kupitia Waziri wa OR-TAMISEMI kwa kuelekeza marejeo ya rufaa za wagombea walioenguliwa katika kugombea nafasi zao. Pamoja na jitihada hizo tunapenda kukumbusha mambo yafuatayo;

i. **Uhakiki wa Daftari la Wapiga Kura:** Tunasisitiza mamlaka kufanya uhakiki wa daftari la wapiga kura ili kuhakikisha wananchi wote wanaopiga kura wana sifa stahiki.
ii. **Uangalifu kwa Kuenguliwa kwa Wagombea:** Tunaomba masuala madogo ya kiufundi yasitumike kama sababu kuu ya kuwaengua wagombea, ili kutoa haki sawa kwa wagombea wote. Kwa kuzingatia kauli ya Mhe. Waziri OR-TAMISEMI tunahimiza wasimamizi na watendaji katika ngazi zote kuzingatia maelekezo hayo bila hila na kwa weledi mkubwa hasa kwa kuzingatia 4R's za Mhe. Rais wetu.
iii. **Mchakato wa Kurudisha Fomu:** Tunapendekeza kuwe na uwazi na urahisi katika mchakato wa kurudisha fomu za wagombea. Hasa ikizingatiwa kuwa Mhe. Waziri wa OR-TAMISEMI ametoa maelekezo ya kuongeza siku 2 za kupokea rufaa, tunatoa rai kwa ofisi kuwa wazi, kusikiliza na kufanya marejeo ya fomu za wagombea kama ilivyoelekezwa.
iv. **Wasimamizi wa uchaguzi:** Tunatoa wito wa kutekeleza majukumu yao kwa uwazi, usawa kwa kuzingatia sheria zilizowekwa bila upendeleo wa aina yeyote. Tunatumia fursa hii kukemea na kuitaka Wizara husika kuwachukulia hatua pale inapothibitika wasimamizi hawa wamefanya kwa makusudi au kwa uzembe. Hii itasaidia kurejesha imani kwa wananchi.
v. **Kampeni za Wagombea:** tunahimiza kwa mamlaka na vyombo vyote vinavyohusika kutoa wigo sawa kwa vyama vyote vya siasa vinavyogombea kufanya Mikutano yao kwa uhuru na usawa bila kubughudhiwa.
vi. **Kuhesabu na kujumlisha kura:** Tunapenda kuhimiza viongozi na wahusika wote kudumisha uwazi katika hatua hii muhimu kwa kuzingatia sheria na kanuni zilizowekwa bila upendeleo wowote ili kudumisha amani baada ya uchaguzi.

vii. **Kutangaza matokeo ya Uchaguzi:** Tunahimiza mamlaka husika zizingatie usawa na uwazi katika kutangaza matokeo halisi ya uchaguzi kwa kuzingatia muda bila ucheleweshaji wowote ambao mara nyingi hupelekea kukosekana kwa Imani na matokeo husika.

CCT inasisitiza umuhimu wa uchaguzi huu kusimamiwa kwa haki na usawa. Hata hivyo CCT inapongeza jitihada za mamlaka kuhakikisha mchakato unafanyika kwa uwazi. Pia tunasisitiza umuhimu wa chaguzi zote kusimamiwa na Tume Huru ya Uchaguzi na pia marekebisho ya katiba ili kuondoa changamoto zinazoathiri mchakato wa uchaguzi kila wakati nchi inapoingia katika chaguzi. Tukumbuke mwakani (2025) tutakuwa na uchaguzi mkuu, hivyo kama hatutachukua hatua stahiki tutakuwa na changamoto hizi hizi katika chaguzi zijazo.

CCT inaendelea kuvikumbusha vyombo vya dola kuwa hatutaki kuona yale yaliyotokea Uchaguzi wa mwaka 2019/20 yakijirudia tena mwaka huu. Ikumbukwe kwamba Watanzania wana haki ya kugombea nafasi za uongozi na kuwachagua viongozi wanaowataka bila shinikizo lolote. Haki hizi zisikanyagwe.

**Ndugu Mwananchi,**

**"Kura yako ni sauti yako! chagua viongozi wanaowajibika na kusimamia uwazi na Utawala Bora" TUWAJIBIKE**

*"Haki huinua taifa; Bali dhambi ni aibu ya watu wo wote" Mithali 14:34*

**Mungu aibariki Tanzania na atupe uchaguzi wenye Haki, Amani na manufaa kwa Taifa letu na watu wote!!!**

**Imetolewa na:**

*Signedtoday14.11.2024*
Askofu Dkt. Fredrick Shoo
**Mwenyekiti wa CCT**

Kwa niaba ya Kamati ya Utendaji ya Jumuiya ya Kikristo Tanzania